# IDARA YA UWAKILI (NETC)
# MPANGOKAZI WA IDARA
# 2017-2020

"**Nayaweza mambo yote** katika yeye anitiaye nguvu."
Wafilipi 4:13

MUNGU KWANZA

## Njozi Yetu

Kila mshiriki kuimarisha tabia ya kumfanya Mungu Kuwa wa Kwanza katika vyanja zote za maisha.

## Utume Wetu

Kuwasaidia viongozi na washiriki kujenga tabia zinazopelekea Makuzi ya Kiroho na Uaminifu katika uwakili

## Shabaha Yetu

Kwa kutambua kwamba uwakili wa Kikristo ni jambo pana sana, na kuwa ni nadharia muhimu inayogusa kila sehemu ya maisha mtu aliyejitoa kwa Kristo - kuanzia mahusiano ya kifamilia mpaka kanuni za kiafya, na kuanzia utunzaji wa muda mpaka utunzaji wa mazingira;

Kwa kutambua kwamba, kuhimiza uaminifu katika nyanja zote hizo ni kazi kubwa isiyoweza kukamilishwa na Idara moja peke yake;

Kwa kutambua kuwa, tofauti na madhehebu mengine, Kanisa la Waadventista wa Sabato limezipatia Idara nyingine kusimamia karibu kila kipengele cha Uwakili (kama vile, Idara ya Afya, Idara ya Vijana, Idara ya Shule ya Sabato & Idara ya Huduma Binafsi na Huduma za Familia);

Idara ya Uwakili, kwa sababu hizo, itasimamia (bila kuacha vipengele vingine vya uwakili) kwa sehemu kubwa mambo makubwa matatu:

01. Jinsi ya Kumtumaini BWANA
02. Uaminifu Maishani
03. Dhana ya Umishonari wa utume kupitia Amana kwa njia zifuatazo:

# UTEKELEZAJI: KATIKA MAKANISA

| | KUKUA KIROHO | KUKUA KATIKA MALEZI | KUKUA KATIKA UFAHAMU |
|---|---|---|---|
| **GOLI LETU** | 100% ya washiriki kufanya upya maagano na Mungu kupitia kadi za Mungu Kwanza, katika wakati wowote hasa katika Sabato za Uwakili kabla ya Mwezi Disemba. | Kuongeza watoaji wa Zaka kufikia asilimia 100% ya watoaji wa zaka 2018. | Kuongeza matoleo ya Sadaka kufikia asilimia 10% ya Wastani wa pato la Mshiriki. |
| **UTEKELEZAJI** | Kujenga tabia ya kiroho, ya Kuwa na Ibada mahususi, kwa mtu binafsi, familia na Kanisa. Washiriki watafundi-hwa namna ya kufanya Ibada za maombi binafsi na kujifunza Biblia kupitia kwa program ya Revived by His Word na Waaminini manabii Wake | Kufanya Program ya Nyumba kwa Nyumba, ambapo Wachungaji na Wazee wa Makanisa wata-chukua wajibu wao wa kiroho wa kuwatia moyo washiriki ambao bado hawajaanza kumumfanya Mungu kuwa wa Kwanza. | Kufundisha Dhana ya Kumtegemea BWANA, Katika muktadha wa utoaji wa Zaka na Sadaka kwa Mpango na bila Kukoma. Kuwahimiza washiriki kukumbuka umuhimu wa Kadi za Mungu Kwanza. |
| **SABABU** | Utafiti umeonesha kwamba: wale walio na tabia ya kurudis-ha kwa uaminifu Zaka ndio hao-hao ambao wanahudhuria Ibada mara kwa mara, wanao-soma Biblia na Miongozo (Lesoni) ya kujifunza Biblia (McClever, 2016), na pia ndio hao ambao kwa sehemu kubwa wanamwamko na wamejitoa kwa kazi za kimishenari. | Kama utoaji wa Zaka na Sadaka unavyoweza kuwa kipimo cha ukuaji wa kiroho, vile vile kutokutoa Zaka na Sadaka unaweza kuhesabika au kuashiria hatua za kuele-kea katika uasi. | Sadaka inawakilisha utayari wa mtu katika suala zima la utoaji wa mpango. Uhalisia unatuone-sha kuwa si kila Mtoa Zaka ni Mwaminifu katika Sadaka. [Kwa maana nyingine, si watoaji wa Zaka wote wanaotoa Sadaka kwa mpango], hata hivyo wanaotoa Sadaka kwa mpango unaozingatia % kwa sehemu kubwa wanakuwa waaminifu pia katika matoleo ya Zaka. |
| **NJIA YETU** | Kila tukio linalohusisha utoaji wa Elimu ya Uwakili wa Kikristo kwa Washiriki, litahitimishwa kwa mwito wa kujiweka wakfu, kupitia kadi za Mungu Kwanza. | i) Mikutano/makongamano yote ya Kiuwakili yatafanywa ili kuwafundisha na kuwatia moyo Wachungaji na Wazee wa Makanisa kujihusisha katika program ya kuwatem-belea washiriki.<br>ii) Kuwatembelea washiriki wote ukiwa na "Agenda Maalum ya Kutembelea" ukianza na wale ambao kwa sababu flani hawatoi Zaka. | Mahubiri yanayofanywa na Wachungaji, Semina za Usimamizi wa Mapato kwa Familia na Makongamano ya Kiuwakili, vitafanyika na vyeti vitatolewa kwa wale watakao-fanya vizuri. |
| **THATHIMINI** | Kulinganisha asiliamia iliyofikiwa kwa washiriki kufanya upya maagano na Mungu Wao. | Kukusanya takwimu makini zinazoonesha taarifa ya watoaji wa Zaka na Sadaka (Kimtaa) ili kutambua uhalisia wa watoaji wa Zaka waaaminifu | Matumizi ya Jicho la Kanisa yatatusaidia kujua maendeleo ya mafanikio katika program hii ya Mungu Kwanza. |

Mpangokazi huu umetengenezwa GC na kuwekwa katika muktadha wa NETC na Almodad Amos.

MIPANGO NA MIKAKATI KWA VIONGOZI

**1. Programu za Mafunzo endelevu, inayofanywa na Viongozi wa Idara ya Uwakili.**

Mafunzo haya maalum yanatakiwa kufanywa na Ofisi za NETC. Taasisi yoyote isyowapeleka watendakazi wake kupata semina ndogo ndogo za mafunzo zitapelekea utendaji kudorola na kazi kufanywa katika ubora wa chini na mazoea yenye matokea dhaifu katika utendaji.

TUWE NA: Retreat za Wachungaji tu, angalau kwa siku mbili ili kufaya tathmini ya utendaji wetu.

**2. Taarifa za mara kwa mara kuwafikia Wachungaji na Washiriki.**

a) Kipimo kinachotumika kwa kufanya tathmini.
b) Asilimia za watoaji wa zaka kwa kila mwezi
c) Asilimia ya watoaji wa sadaka kila mwezi
d) Kupima wastani wa Zaka kwa kila mshiriki (Kwa ngazi ya Konferensi)
e) Kiwango cha ukuaji kwa kila kipengele hapo juu, tangu taarifa iliyopita

Mkurugenzi wa NETC kuipima mitaa, Wachungaji kuyapima makanisa, Wazee kuwapima Washiriki.

**3. Uwazi na Uwajibikaji wa Viongozi**

a) Maidara yote kuwajibika kutoa taarifa ya nini wanafanya. Uongozi kuwa na wazi wa kiasi cha zaka na sadaka iliyotolea na jinsi inavyotumika.
b) Matumizi ya Media (Vyombo Stahiki vya habari) katika kutoa taarifa ya mapato na matumizi kila mwisho wa mwezii.
c) Kukaza sana habari ya Udhibiti wa mali ya BWANA
d) Kukazia mfumo mzuri wa utoaji wa matoleo ikiwemo ukataji risiti na matumizi ya njia za kisasa katika kupokea matoleo.
e) Kuwatia moyo washiriki kuhakiki risiti walizoandikiwa na kuziomba bila kuona aibu.

**4. Uendeshaji Mzuri wa Ibada ya Matoleo Yenye Kicho na Tafakuri Njema Kanisani**

Kuhimiza ibada zilizo bora na utaratibu mzuri wa ibada ya matoleo inayoongozwa kwa ustadi mzuri, utakaowafanya waabuduo kuona maana ya Ibada ya matoleo.

Kufanya Ibada za majuma ya uwakili yaliyopangiliwa vizuri na kuwekewa malengo mahususi.

**5. Kuhimiza Utoaji wa Mpango**

Viongozi wajihusishe kutambua changamoto na sababu zinazowafanya washiriki kutokutoa kwa mpango na kuwasaidia aidha kwa kuwatia moyo au kujibu dukuduku zao.

**6. Mikutano na Makongamano ya Kiuwakili**

Idara ya uwakili iandae mafunzo maalum kwa wachungaji, wazee wa makanisa na wakurugenzi ili kuojielimisha na kufanya maagano upya ya kumtumikia Mungu, mara kwa mara.

**7. Kujifunza Theolojia ya Uwakili**

Kuwafundisha washiriki kuelewa maana halisi ya uwakili na jinsi unavyoathiri mustakabali wa Maisha ya Kikristo.